

Sipangwingwi, Watajua Hawajui: Jaribio la Kuelekeza Matumizi ya Lugha Dhidi ya Uhalsia wa Kiisimujamii

Samuel M. Obuchi¹ na Nabeta K. N. Sangili²

¹Chuo Kikuu cha Moi

²Chuo Kikuu cha Kaimosi

Ikisiri

Makala haya yanaangazia nyimbo mbili, ‘Sipangwingwi’ na ‘Watajua hawajui’ ambamo mnapatikana maneno mawili *Sipangwingwi* na *Watajua hawajui*. Hivi karibuni, Serikali ya Kenya, kupitia Shirika la NCIC imetoe tamko ambalo linaharamisha matumizi ya haya maneno mawili, mionganoni mwa mengine kwa madai kwamba huenda yanaweza kuibua hisia fulani ambazo zinaweza kuchangia hali ya machafuko katika na baina ya Jamiumizi lugha mbalimbali. Makala haya basi yanajadili matumizi ya vifungu hivi viwili kwa kurejelea nyimbo hizo mbili ambapo waandishi wamejaribu kuonyesha kwamba ni makosa kuelekeza matumizi ya lugha, kwa kuwalazimisha wanajamii kutotumia maneno fulani ambayo, huenda yanatumiwa kwa wingi na mtu au mwanasiasa fulani. Ukweli wa kiisimujamii ni kwamba, lugha inafaa kujiendezea, kujikuza na kujisambaza kote, kutegemea watumiaji wake, katika muktadha wowote: sokoni, kanisani, msikitini, mtaani, na kwingineko.

Maneno Muhimu: Sipangwingwi, Watajua, Hawajui

Utangulizi

Kulingana na Iribi (2011), kila lugha inayotumiwa na binadamu hubadilika kila uchao na hivyo, lugha yoyote, kwa mfano Kiswahili, imekuwa ikibadilika kihistoria na ingali inaendelea kubadilika. Anatoa kauli kwamba kwenye kamusi yoyote ile ya sasa upo uwezekano kuwa kutapatikana neno UKIMWI kinyume na ilivyokuwa kwa kamusi zilizoandikwa miaka ishirini iliyopita. Kutohana na maelezo haya, tunaweza kudai kwamba: **Sipangwingwi, Watajua hawajui** ni maneno ambayo, yameanza kutumiwa kwa wingi sana katika mazungumzo ya kawaida, vilevile ya kisiasa nchini Kenya. ‘**Sipangwi**’ ni kinanusho cha kauli yakinishi, ‘**nitapangwa**’, ambapo ‘**Watajua Hawajui**’ ni maneno ambayo yanatumika siku zote katika Kiswahili sanifu. Lakini katika siku za hivi karibuni, maneno hayo, ambayo yameanza kutumiwa kwa pamoja (**watajua hawajui**) yameibua hisia fulani zenye kuonyesha misimamo mikali katika taaluma ya siasa, nchini kenya. Kwa mantiki ii hii, tunaweza kusema kuwa Kiswahili, sawa na lugha nyingine za kilimwengu, zitaendelea kubadilika.

Uelekezaji wa Lugha katika Jamii

Lugha ipo kwa ajili ya binadamu. Na binadamu huyu ana uhuru wa kuitumia lugha yake kwa maslahi yake na ya wenzake. Hata hivyo, kutohana na kuwepo kwa mifumo ya utawala na serikali, suala la kuelekeza jamii jinsi ya kutumia lugha limekuwepo kwa muda mrefu katika jamii. Lengo kuu la kuelekeza matumizi ya lugha aghalabu ni kuleta amani na kuzuia mtafaruko unaoweza kuzuka iwapo kila mwanajamii anaweza kusema atakavyo na chochote atakacho. Kwa mujibu wa Bhadani (2013) mzozo wowote unaozuliwa na binadamu akimlenga binadamu mwenzake huchochewa kupitia kwa lugha au uteuzi mbaya wa maneno wakati wa mawasiliano. Anazidi kusema kwamba binadamu huhisi vibaya anapotukanwa kupitia kwa maneno maalum kiasi cha kuamua kupigania kimwili hadhi yake. Kwa maoni yake, neno linapopewa maana na walengwa, wao ndio huamua kiwango cha mzozo au vita. Hii ndio sababu kubwa utawala katika vipindi tofauti tofauti vya kihistoria vimekuwa vikijaribu kudhibiti matumizi ya lugha au maneno mahsusii.

Kulingana na Ong (1982) kadiri dunia inavyosongea katika kizazi cha teknolojia na utalifa wa kimawasiliano, maarifa na habari huzidi kusambaa na kuzua mwamko wa kitabaka. Matabaka haya

hukuzwa katika kiwango fulani cha kimsamiati na msamiati huo unapotumiwa katika harakati za kisiasa, kidini au kwa namna nyingine, ari ya kupigania haki zao huwa ya kiwango cha juu. Hivyo, ari hii inaweza kugeuka kuwa vita vya kijamii, kidini au kimataifa. Hii ndiyo sababu kubwa ya baadhi ya serikali na tawala kupanga lugha au kuelekeza maarubu ya lugha mahsus, ikiwemo kupiga marufuku matumizi ya maneno fulani katika jamii. Licha ya kwamba pana juhud za kudhibiti lugha na matumizi ya msamiati fulani fulani, wanaismujamii wanapinga hatua hizi kwa sababu zinazuia maendeleo ya lugha. Aidha, tafsili ya maana ya neno hutegemea saikolojia na muktadha. Hii ndiyo sababu neno lilo hilo linaweza kukubalika katika muktadha mmoja kutokana na jinsi wahusika wanavyolijengea maana na kwa upande mwingine, neno hili likapigwa marufuku kutokana na jinsi watawala, viongozi wa kidini au serikali inavyodhani linafasiliwa na wanajamii kwa kipindi fulani. Hii ndiyo sababu Muji na Wahyu (2017) wanashikilia kwamba ni vigumu kuwekea sera au sharia za kudhibiti au kupiga marufuku matumizi ya msamiati maalumu. Wanatoa sababu zao kwa kudai kwamba suala la maana ni suala la kisaikolojia na haiwezekani kuunda sharia au sera jinsi watu watafikiria na kufasiri maana. Hii ni sawia na utawala au serikali kufikiria kwa niaba ya wanajamii-lugha. Hii ni sawia na kuweka maneno katika makundi ya miiko na tasfida, kwamba hayafai kutumika hadharani kwa sababu yatazua hisia fulani mionganoni mwa wanajamii (Trudgill, 2002; Wardhaugh, 2002).

Kwa mujibu wa wanaismu wa forensiki, mifumo mbalimbali ya kimtandao imekuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza maneno fulani yanayoweza kuzua mizozo ya kijamii, kidini au vita bayana ya mataifa (Mahony, Albrecht na Sensoy, 2019). Kuchemka kwa mizozo ya *Arab Spring*, vita vya kisiasa vya baada ya uchaguzi nchini Kenya, vita vya Nigeria kwenye oil Delta na maandamano ya Black Lives Matter kulifanikiwa kwa sababu ya maneno machache yaliyowasha mizozo na maandamano katika mataifa na dunia nzima. Hii ndiyo sababu Cedeman na Nils (2017), Ceron na wenzake (2017) na Chadefaux (2014) wanashikilia kwamba ni rahisi utawala au serikali kuititia kwa teknolojia ya kisasa kukisia machafuko katika jamii kwa kuangalia jinsi msamiati fulani unatumwiwa katika jamii kwa kipindi maalumu kama vile cha kisiasa na kidini. Serikali inapohisi kwamba msamiati fulani uliwahi kutumika awali katika historia ya jamii na baadaye ukasababisha maafa, mizozo au vita, basi msamiati huo unapigwa marufuku na serikali kuchukua hatua ya kudhibiti na kuamua jinsi wananchi watatumia lugha na maneno maalumu kwa kipindi fulani. Kwa hivyo, Kenya, kama yalivyo mataifa mengine ulimwenguni kama vile Marekani, Ujerumani nakadhalika, yameingia katika kipindi cha kupiga marufuku msamiati, japo haikutolewa idhibati yoyote ya kisayansi au kihistoria kwa baadhi ya maneno yaliyowekwa kwenye farahasa ya marufuku hii. Sehemu inayofuata inaonyesha baadhi ya maneno ambayo yalipigwa marufuku na kudai kwamba NCIC haikuzingatia historia ya kisiasa katika kutekeleza hatua hii ya kimhemko.

Sipangwingwi na Watajua Hawajui: Uhaliwa wa Kiisimujamii

Tarehe nane mwezi wa Aprili, 2022, NCIC, kuititia mwenyekiti wake, Rev. Dkt. Samwel Kobia alianda kikao na wanahabari kwa lengo la kuarifu taifa kuhusu maneno yaliyokuwa yanapigwa marufuku kuanzia huo wakati. Baadhi ya maneno yaliyopigwa marufuku ni pamoja na *Kaffir* (lenye kutoholewa kutoka lughaya kiarabu: *Kafir* lenye maana ya mtu asiyeamini na mwenye kuuficha ukweli) *madoadoa, chunga kura, mende, watu wa kurusha mawe, watajua hawajui, wabara waende kwao, wakuja, Chinja Kafir*, na *kwekwe*. Kwa kiasi kikubwa, haya ni maneno yanayotumiwa katika lugha ya Kiswahili. Pia maneno yenye kutumiwa kwa wingi zaidi katika Sheng, hayakushazwa. Maneno hayo ni pamoja na:

Kama noma noma, kama mbaya mbaya (*japo ni maneno ya Kiswahili*)

Hatupangwingwi
Operation Linda Kura

Lugha ya Kikuyu, nayo imepunguziwa msamiati wake. Ni marufuku basi kutumia maneno yafuatayo:

Kihii (ambaye hajapitia sherehe ya jando)
Uthamaki ni witu (utawala/uongozi ni wetu)
Mwiji (Kimeru) (*ambaye hajapitia sherehe ya jando*).

Shirika la NCIC kupyitia mwenyekiti wake linadai kwamba matumizi ya maneno haya katika taaluma ya siasa huenda yakaigawanya nchi zaidi kwenye misingi ya kikabilo; kwamba maneno haya huenda yakachangia au yakachochea fitina, uhasama, vita na machafuko ya kisiasa. Hivyo, ni marufuku kutumia maneno haya katika diskosi ya kisiasa, kwa kuwa inaaminika kuwa yanasheneni maana fiche, ya ndani kwa ndani, maana ambayo inaeleweka kwa wanaoitumia tu.

Sababu kuu inayodokeza katika kuikuza kauli hii ni kwamba huenda yakapelekea machafuko sawa na yale yaliyoshuhudiwa nchini Kenya kufuatia uchaguzi tatanishi uliofanyika nchini 2007/8, ambapo watu wengi sana waliuawa. Bwana Kobia aliendelea kudai kwamba mirengo ya kisiasa yenye kutumia maneno haya kwa wingi ni: *Kenya Kwanza Alliance*; na *Azimio La Umoja*. Kinachomtia hofu zaidi ni kwamba maneno haya yameelekeea kutumiwa kwa wingi zaidi katika mitandao ya kijamii ambayo huwashirikisha watu wengi na makundi mengi mno ya kijamii. Makundi haya ya kijamii hujitokeza zaidi kwenye: *Facebook, Twitter, YouTube* na WhatsApp:

Maisha ni yangu, we shughulika na yako
Napenda za kwango, we shughulika na kwako
Mi sipangwingwi, sipangwingwi
Mi sipangwingwi, sipangwingwi
Mi sipangwingwi, sipangwingwi
Mi sipangwingwi, sipangwingwi

Katika kifungu hiki, mwimbaji anaelekeea kutumia maneno kiufundi ili kupyitisha hoja kwamba **anahangaikia hali yake** (maisha ni yangu) huku akiwashauri wasikilizaji wake wasiwe na haraka ya kuyaingilia maisha yake (shughulika na yako). Kifungu hiki kinashadidia kauli kwamba kila mtu ana haki ya kufanya maamuzi ambayo yanamhusu, na kwamba yejote hana haki ya kumuungilia. Hili ni neno la sheng lenye maana kuwa yejote hana ruhusa wala hatarajiwi kukuelekeza kwenye mkondo wa maisha usioupenda. Shirika la NCIC linaelekeea kuielekeza jamii-tumizi lugha inayokisiwa kuwa imekuwa uongozini kwa muda mrefu sana. Walioelekea kulengwa zaidi ni jamii ya Wakikuyu na Waluo. Naye Linus Kaikai ambaye ni mwanahabari mashuhuri anatoa maeleo kwamba walipoanza kutumia maneno **hustler** na **Dynasty**, hamna aliyejitokeza kukashifu matumizi ya maneno haya mawili. Mwende (2022) katika gazeti la *The Star* anadai kwamba neno hili lilitumiwa na Mhesh. Ruto, ambaye ni kinara wa *Kenya Kwanza Alliance* kuzindua kampeni zake za Urais na lengo lake kuu lilikuwa ni kudai kwamba watu wachache hawawezi kuamua nani atakuwa Rais wa Kenya. Mwende akinukuu Mhesh. Ruto, “vile Wakenya wamesema, hawapangwingwi, na mimi nataka niwaambie, mimi pia kama hustler sipangwingwi...wao wanaweza kupangwa na deep state system lakini sisi hatupangwingwi”. Msanii Tony Kinyanjui (Exray) anadai kwamba wimbo huu haukutungwa kwa nia ya kisiasa. Alitunga ili kuwajibu watu waliokuwa wanamuuliza atatunga tena wimbo wake lini baada ya wimbo wake na Mejja wa “Usherati”. Hivyo, katika kuwajibu, alisema, “*nitatoa ngoma siku ile nataka; so sipangwingwi.*” Hivi ndivyo wimbo huu uliibuka Oktoba, 2021 na baadaye kusambaa katika siasa. Kwa hivyo, kupewa maana ya kisiasa si wazo la msanii bali jinsi mashabiki/wanasiasa walivyouchukua na kuingiza katika muktadha wa kisiasa. Wimbo huu, ambaou ulikuwa wa kufurahisha moyo wake, ulichukua maana ambayo Dkt. Kobia anasisitiza kwamba, “neno sipangwingwi lina vipengele vya matamshi ya chuki dhidi ya familia na jamii ambazo zimekuwa katika mamlaka ya taifa kwa muda mrefu. Jamii ambazo zinarejelewa ni za Luo na Kikuyu.” Hii ndiyo sababu Ong (1982) anadai kwamba ni vigumu kuwekea sharia au sera fasili/maana za maneno kwa sababu kila mmoja au kundi la watu wanafasili tofauti na wenza. Hivyo, kiisimujamii, huku ni kama kulazimisha jamii ifikirie na kutumia msamiati fulani kwa mujibu wa dola za serikali inayotawala au jinsi kundi moja lingependa. Aghalabu, ufikiriaji huu huegemea kufurahisha upande wa serikali tawala. Katika kifungu kinachofuata, tunapata:

Unataka mtu simple humble, rich young
Ndo upeane namba
Unataka mtu mdark, mlight mtall
Babe tafuta wababaz
Unaplan future yetu kumbe uko alone
Maisha ni safari mi na ride along
Labda mi niomoke nikuitage form...
Ama labda we uomoke nikujage home
Mi nayo pombe siwezi onja
Aiii nakunywa yote
Na akiamua kukupatia
Aiii chukua yote

Katika hiki kifungu, msanii anaandama kauli yenye kulenga **mapenzi**. Ilivyo ni kwamba anaelekea kumkashifu mwenzake ambaye ana muelekeo tofauti na wake. Anamwona mwenzake kama asiyefuata dira salama yenye kuja mapenzi ya kikweli na ya hakika. Ndiposa anamwambia:

Unataka mtu simple humble, rich young
Ndo upeane namba
Unataka mtu mdark, mlight mtall
Babe tafuta wababaz

Ni wazi kuwa msanii hayuko tayari kuingiliana kimapenzi na mtu ambaye anahitilafiana naye kimaisha. Hivyo, hayuko tayari kuingiliana na mtu wasiyeelewana. Kwa kweli, kauli hii ya kutaka kuishi maisha yake, apendavyo. Anasema:

Maisha ni yangu, we shughulika na yako
Napenda za kwangu, we shughulika na kwako
Mi sipangwingwi, sipangwingwi
Mi sipangwingwi, sipangwingwi
Mi sipangwingwi, sipangwingwi
Mi sipangwingwi, sipangwingwi

Kifungu hiki kimeweka wazi kauli ya msanii kuwa hayuko tayari kuelekezwa, kupangwa na kufanyiwa maamuzi. Ni kutohana na hali hii ambapo anarudiarudia neno: **Mi sipangwingwi, sipangwingwi**. Hili si neno la Kiswahili. Kuna uwezekano kuwa linalekeea kutumiwa zaidi katika lugha ya SHENG'. Kwa kuwa linaludiwarudiwa, tunaweza kudai kwamba linaashiria msisitizo wa msanii kuwa kwa vyovoyote, abadan kataan, hayuko tayari kuelekezwa na mwenzake na wala kufanya mambo jinsi wao wanataka yeayatekeleze. . Katika kifungu kifuatacho, mwimbaji anasema:

Mi sipangwingwi, kijana ni gwiji
Utapangaje morio ana kashilingi kwa wingi
Mafeelings za nini mi ni jangili kamili
Nasuka mamdenge za matajiri wa mjini, samahani
Chai fupi nmejaza maziwa na majani
Sikusuki mi ni Trio Mio watagwan
Ka hunijui unajifanya bombo haja gan
Abiria nawapanga ka makanga wa Kasaran
Ama vijiti za viberiti ndani ya boxdem
Wanga stishiki naget mabinti nawachokdem
Washa ngwariti tuskie fiti adi shokdem
Cheza na mangoksdem

Kifungu kilichonukuliwa hapo juu kinamdhahirisha msanii kama mwenye majisifu mengi. Hebu rejelea kauli zilizoandikwa kwa wino uliokolezwa:

Mi sipangwingwi, kijana ni gwiji
Mafeelings za nini mi ni jangili kamili
Ka hunijui unajifanya bombo haja gan
Abiria nawapanga ka makanga wa Kasaran
Ama vijiti za viberiti ndani ya boxdem
Cheza na mangoksdem

Katika kifungu hiki, maneno yaliyopigwa mstari yanalekea kuonyesha kwamba mwimbaji ni mtu ambaye ni: stadi katika mambo yake; mtu asiyejali na hapendi watu wasiomjua kudhani wanaweza kumfanyia lolote la kumtweza; yeze ndiye mwamuzi wa watu wengine na anawapanga apendavyo. Kimsingi, taswira inayochorwa katika kifungu hiki ni ile ya mtu apendaye kuelekeza ila hafai kuelekezwa. Kisha msanii anarudia korasi ileile moja kwa nia ya kusisitiza kauli anayoipalilia moyoni: ***Maisha ni yangu, we shughulika na yako.*** Wanasiasa wa mrengo wa Kenya One Alliance huenda walivutiwa na huu wimbo na maneno yake/maudhui yake kutokana na uhusiano uliodorora wa Rais Kenyatta na mwendani wake Mhesh. Ruto, ambaye ni Naibu wake wa Rais. Maudhui ya wimbo huu yanapata mashiko hasa katika mrengo huu kutokana na maridhiano kati ya Kinara wa NASA, Mhesh. Raila na Rais Kenyatta. Kinara wa *Kenya One Alliance* alihisi kwamba alikuwa anapangwa na viongozi hawa wawili na ndio maana pakawa na haja ya yeze kutafuta njia mbadala ya kuwania Urais. Wimbo huu, kwa hiyo, unapata maana mpya katika muktadha huu wa kisasia.

Katika kifungu kinachofuata, msanii anaendelea kujisifu kwa kujilinganisha na wanyama kama vile **chui**. Anadai kwamba yeze ana usiri usioleweka na wala hafai kueleweka. Anasema kuwa wakati wa mchana ana haki ya kuufunika uso wake, huku akiandama njia na mielekeo aipendayo. Aidha, anadai kwamba yeze ni mnyama hatari, ana uwezo wa kuwararua wanaojaribu kuyaingilia maisha yake: **Ukitaka mizuka, mimi ndo hooker; Tena nagwara nikidara nina vikucha; Naishi nitakavyo ondoa vikwazo; Ukiona najidai jua kujikopa ndo chanzo; Nikishika ngiri natesa na majigambo.** Msanii kwa uwazi zaidi ameonyesha jinsi alivyo mkali, kiasi cha kuogopwa na wote wanaojaribu kuyaingilia maisha yake. Aidha, ni mtu asiyetegemea wenzake kifedha na anapopata hela (elfu moja), anabwaga moyo kwa kujinaki. Ni katika muktadha huu ambapo kiongozi fulani wa kisasia alinukuliwa akisema (kwenye **Youtube**) kuwa:

*Wakenya wamesema hawapangwingwi
Mimi pia kama hustler sipangwingwi
Wao wanaweza kupangwa na deep state na system-na sisi pia
hatupangwingwi
Tutatembea pamoja mpaka tufike...tuko na Mungu.*

Tuendelee kuuchambua wimbo wa **hatupangwingwi**:

Aah mi sitambui mbui, mi mchana buibui
Nikiwa mababi mahali leta maruirui
Na niko na mashoga kibao nataka madui dui
Sitaki kifisi niko bongo nasaka chui chui
Ukitaka mizuka, mimi ndo hooker
Tena nagwara nikidara nina vikucha
Hiki kichupa shika na kupa
Na wanapenda ukipapia baba pupa
Naishi nitakavyo ondoa vikwazo
Ukiona najidai jua kujikopa ndo chanzo
Nikishika ngiri natesa na majigambo
Ju naona siku hizi ganji mnasafisha kwa mitambo

Msanii katika kifungu hiki anazidi kusisitiza kwamba mbali na yeze, hapana mwinge aliye mkali kumshinda; kwamba ana marafiki wengi ila sasa anatafuta sana maadui, hata katika nchi jirani ya Tanzania. Anapohitimisha ubeti huu, msanii huyu anaelekea kutaja suala la pesa bandia au biashara ya “wash-wash” (ganji mnasafisha kwa mitambo). Suala la ughushi wa hela limeathiri baadhi ya wanasiasa na wasanii maarufu nchini Kenya japo hakuna hatua madhubuti ambayo serikali

imechukua. Msanii anaукamilisha wimbo wake kwa kurudia korasi aliyoanza nayo. Kifungu hicho kimejitokeza kotekote katika wimbo huu.

Mwimbaji mwingine Khaligraph, anajitokeza na wimbo **watajua hawajui**. Tumeugawa kwenye vifungu kadhaa na kujaribu kuuchambua ifuatavyo: **Wataju hawajui**. Kifungu hiki nacho, kimeibua hisia kali sana mionganoni mwa wanasiasa. Kama tulivyodai mwanzoni mwa makala haya, wanasiasa kwa kiasi kikubwa hupenda kijinasibisha na matumizi fulani ya maneno ambayo huweza kukuza kauli zao. Hata hivyo, katika makala haya, tunaonyesha kwamba maneno haya hayakudhamiriwa kukuza kuendeleza mitazamo ya wanasiasa fulani. Ilivyo ni kwamba, nyingi ya nyimbo hizi huimbwa muda mrefu kabla ya tukio au matukio fulani kutokea. Wanasiasa, kwa mfano, huzisikiliza nyimbo hizi na kugundua kwamba ni malighafi nzuri ya kukuzia sera na matamanio yao. Na kwa kuwa nyimbo hizi huimbwa na kupendelewa sana na vijana, basi wao hupenda kuziimba ikiwa ni pamoja na kutumia maneno fulani yaliyomo kwa lengo la kijinasibisha sio tu na waimbaji husika, bali pia na vijana hao ambaa huzipenda na kuziimba. Hebu sasa tuangazie wimbo: **watajua hawajui**.

WATAJUA HAWAJUI

You all's not ready
Hiyo chopper iko steady
Shot shot everywhere (brr rr rr)
Shot shot on the belly
Umeniona kwenye telly
Me ni kama Balotelli
Flow tight kama virgo
Lakini simaanishi Mary

Msanii amejawa na majisifu mengi. Anajilinganisha na ndege aina ya helikopta (chopper); ndege hiyo iko imara sana (iko steady), haiyumbi na ina uwezo wa kufyatua risasi kwa wingi kwa mahasimu wake (*Shot shot everywhere(brr rr rr) Shot shot on the belly*). Aidha anajilinganisha na mchezaji maarufu Balotelli (Me ni kama Balotelli) aliywahi kuchezea timu ya Manchester City enzi zake. Msanii huyu anadai kuwa bikra japo si kama Maria wa Bibilia. Huenda ubikra wake unatokana na kwamba ndio mwanzo anaingia katika tasnia ya muziki wa kufokafoka.

He take money from you and he brings it back to me
I aint twerit about to pites i'ma sip dis Hennessey
Becoz no kama gonna stuck, blow the kip flikati
We may run up on your back, if you diss the Kale queen
Kale queen, mimi staki drama
Wanapenda vile mimi nachana
Mama we ah nione gah!
Ah mutingonyo, Ah muntungimye
Geba tu wandonyo, kal tu wanjega
Kyal tu an ingwe, ah kye wegega
Kyam tu animye, ai chap bingwe
Age-lu chegaa, am muno chami

Katika kifungu hiki, msanii anaelekea kumdhalilisha hasimu wake. Kwanza, anamkumbusha kwamba yeye ana uwezo mkubwa wa kunywa vileo vyta thamani (**Hennessey**). Anaelekea kumkumbusha kuwa wao wawili hawapo katika ligi moja. Msanii anacheza katika ulingo wa kimataifa, na kwamba hasimu wake anafaa kutosheka na ligi yake ndogo yenye kuchezea maeneo ya sokoni (**Geba tu wandonyo**):

Geba tu wandonyo, kal tu wanjega
Kyal tu an ingwe, ah kye wegega

Japo msanii anatumia maneno mengi yanayopatikana katika lahaja mojawapo ya lugha ya Kikalenjin, ni wazi kuwa ameghadhabika sana kiasi cha kutumia maneno yenye kuzitoa hisia zake

zilizo moyoni. Hisia hizi zinadhihirika vyema zaidi anapotumia luga yake ya mama ambayo ina uwezo mkuu wa kuzidhihirisha kwa wasikilizaji wake.

Kayole to Bomet wanapiga saluti brah!
 Mashore na ma fellow, ma diva, ma groupie... Yeah!
 Papa na Msupa S tushajipa mashughuli... ah!
 So wakijifanya hawajui
 Wakijifanya ndo
 Watajua hawajui... Eh! (Khaligraph)

Katika kifungu hiki, msanii anaendeleza majisifu yake binafsi. Anasema kuwa amejilimbikizia sifa lukuki (**Kayole to Bomet wanapiga saluti brah!**) na kuwa anayejifanya halijui hilo, basi anajidanganya na kwamba atakuja kustaajabu (**So wakijifanya hawajui**). Kifungu kinachofuata kinaendelea kuisisitiza hoja kuwa msanii ni hodari katika taaluma yake, na hivyo, wanaodhani kuwa wanaweza kupingana naye wataambulia patupu.

Watajua hawajui (Msupa S)
 Watajua hawajui... Yeah!(Khaligraph)
 Watajua hawajui(Msupa S)
 Watajua hawajui,Buda!!(Khaligraph)
 Watajua hawajui (Msupa S)
 Watajua hawajui.....Jui!(Khaligraph)
 Watajua hawajui.....Jui!(Khaligraph)

Msanii ameendelea kujisifu katika kifungu kinachofuata:

Endolet nimenunu samba
 Nimefungua mbiasala Namanga
 Bibi ndatoa Gatanga, Mahali ndalipa kama lolo atalamba
 Mimi ni lafiki ya Luto
 Ju ye ndio hunisikia mfuko
 Msupa aliniso wakale wanapesa nikasema ntapitia huko
 Now lets get back to reality

All of this niggaz you stopping, I might have to get on a track wth the queen

Girl you're a G an' I'm lovin your confidence

And on the real, You're on your level

I love how you pushin your feet on the pedal

Na mbona mnajifanya hamjui pia me ni mkale?

Why do you think they call me Julius Yego?

Ka ni Buzz mimi ni baba Kamiti

Jeshi ka kura za Tharaka Nithi

John Snow, kwa hii game of thrones

Ju mikono zangu ndio zina dara Khaleesi

Me ni msee wa kismaat, para sina

Swara sina na hasara sina

ukitaka ata unaeza uliza Sara Amina

nina hype kama ile movie ya Sarafina

Nilijua tukifanya hii collabo hii industry tutaimess

Ju track tunaipiga na kale na ina come na mzuka fresh

So next time you see me salute me ju me ndo the buda yesss!

Unadhani utaezana na OG akikuja na Msupa S

Huyu msanii anatoa mifano mbalimbali inayoifafanua hali yake ya utajiri. Anaema kuwa amenunua shamba/samba kule Eldoret, amefungua biashara Namanga, na kwamba ana uhusiano wa karibu na Luto (hatuna uhakika anayemrejelea hapa!), japo tunakisnia kuwa pengine huyu ni kiongozi mashuhuri na mwenye ushawishi mkubwa nchini. Aidha, anajilinganisha na watu mashuhuri

mbalimbali (...track with the queen, ... pia me ni mkale...; *Why do you think they call me Julius Yego? ...; John Snow, ...; Me ni msee wa kismaat, ...; Sara Amina* nina hype kama ile movie ya Sarafina. Ni kutokana na sifa hizi anazojilimbikia ambapo anatoa onyo kali kwa mhasimu wake (asiyejulikana kuwa asijaribu kujilinganisha naye (*So next time you see me salute me ju me ndo the buda yesss*). Na kama anavyodai katika kifungu kifuatacho, ulimwengu mzima umeamua kumpigia saluti, tangu Kayole hadi Bomet. Katika hiki kifungu, msanii anafikiri kuwa sifa zake zitaendelea kusambaa kote na hakuna uwezekano wa sifa hizo kuyeyuka. Hebu rejea maneno yaliyopigiwa msitari:

Wakidhani ndarudi chini, watajua hawajui!
Me nirudi chini bado, watajua hawajui!
Naenda mbele bado, watajua hawajui!

Kifungu hiki kifupi kinadhihirisha msanii aliyejamini katika kile ambacho anatenda na maisha anayoishi. Maisha haya, wapinzani wake wanatarajia yatasambaratika na kurudi chini ila ye ye mwenyewe anadai kwamba wao hawajui uwezo wake. Katika kifungu hiki, msanii anayahitimisha majisifu yake kwa kussitiza hoja kwamba watu wote, kutoka hapa na pale washamtambua kuwa ye ye ni jogoo linalowika vijijini na mjini pia; kwamba wasiolitambua hilo waanafaa kutambua ukweli kuwa, mwishowe, **watajua hawajui**.

Kutokana na wimbo huu ultiotungwa mwaka wa 2018, ni wazi kwamba wasanii hawa hawakuwa na nia ya kuzungumzia siasa wala utawala. Lengo la wimbo wao lilikuwa ni kufurahisha hadhira yao kwa wimbo wa majigambo, sanaa ambayo ni ya kawaida katika fasihi simulizi. Hata hivyo, wanasiasa wamechukua wimbo huu, hasa kibwagizo watajua hawajui na kukipa maana ambayo, NCIC wanaamini ni hasi na ya kuleta fujo au machafuko ya kisiasa. Kulingana na Dkt. Kobia, walitumia kigezo cha kihistoria cha kuchunguza jinsi wanasiasa walitumia msamiati katika kusababisha ghasia na machafuko. Baadhi ya maneno ambayo Mahony, Albrecht na Sensoy (2017) wanarejelea kuwa na historia ya uchochezi kisiasa na ndio hayo Dkt. Kobia arejelea ni kama vile kihii, kwekwe, madoadoa nakadhalika.

Kulingana na maoni ya rais wa Shirika la Wanasheria la Kenya (LSK) bwana Eric Theuri, shirika la NCIC halina uwezo wa kuainisha maneno kama ya kuchochea ghasia au matamshi ya chuki. Anadai kwamba muktadha ambamo neno linatumwa huwa muhimu sana, hasa kuhusiana na uchochezi na matamshi ya chuki (Kagonye, 2022). Katika mahakama ya kisheria, ni vigumu kudhibitisha kwamba watu walipigana kwa sababu ya maneno. Watu aghalabu hupigana kwa sababu ya rasilimali, kutengwa kisiasa, kijamii au hata kidini ila ni vigumu lugha kuwa sababu kubwa ya machafuko yoyote yatokeayo katika jamii. Japo kuna maneno ambayo yalitumika kuzua vurugu za kisiasa mwaka wa 2007/2008 na yameharamishwa na NCIC, maneno mengine kama vile Sipangwingwi, watajua hawajui, linda kura nakadhalika, hayana historia yoyote ya kisiasa na hayajawahi kutumika katika siasa za Kenya. Hivyo, ni vigumu sana kuyaweka katika kundi la maneno yaliyopigwa marufuku.

Hitimisho

Makala haya yamezihakiki nyimbo mbili, **Sipangwingwi na Watajua hawajui** mnampatikana maneno mawili **Sipangwingwi na Watajua hawajui**. Makala yameubainisha ukweli kwamba serikali, wala chombo chochote kile chenye kukusa sera zozote zile, hakipaswi kwenda kinyume na uhalisia wa kiisimujamii. Kauli ya makala haya ni kwamba Serikali ya Kenya, kupitia Shirika la NCIC halikupaswa kutoa tamko la kuhamisha matumizi ya haya maneno mawili, mionganii mwa mengine. Ukweli usiopingika ni kwambakuna visababishi vingi ambavyo vinaweza kusababisha machafuko ya kikabila, kijamii na kadhalika. Makala haya basi yanapendekeza kwamba lugha inafaa kuruhusiwa kutumiwa ipendavyo na ni makosa kuelekeza matumizi ya lugha, kwa kuwalazimisha wanajamii kutumia maneno fulani ambayo, huenda yanatumiwa kwa wingi na mtu au mwansasiasa fulani. Makala haya yanatoa hoja kwamba kuna haja ya kuyatafitia maneno haya mawili, na mengine

kadhaa yaliyopigwa marufuku. Hii ni kwa sababu, uwekaji wa mipaka ya maana kwenye neno ni suala la kisaikolojia na maana hizi hutofautiana kutegemea muktadha. Serikali inapoamulia wanajamii (kwa sera, sharia au tamko) maneno wanayostahili kutumia na yale wasiyostahili huwa basi inadhibiti maendeleo bunifu ya lugha.

Marejeleo

- Bhadani, V. (2013). Towards Understanding Language and Violence. *ELT Quarterly*, June 2013
Issue from H M Patel Institute of English Training and Research, Vallabh Vidyanagar, Gujarat.
- Cederman, L. and Nils, B. W. (2017). "Predicting Armed Conflict: Time to Adjust our Expectations", *Science*, 355(6324).
- Ceron, A. et al. (2017). *Politics and Big Data: Nowcasting and Forecasting Elections with Social Media*, New York: Routledge.
- Chadefaux, T. (2014). "Early Warning Signals for War in the News", *Journal of Peace Research*, 51(1)
- Iribemwangi, P. I. na Mukhwana, A. (2011). Isimujamii, Nairobi: Focus Publishers.
- Kagonye, F. (2022). Storm as NCIC releases list of hate speech words. *The Standard*.
<https://www.standardmedia.co.ke/national/article/2001442707/storm-as-ncic-releases-list-of-hate-speech-words>
- Mahony, C, Abrecht, E. and Sensoy, M. (2019). *The relationship between influential actors' language and violence: A Kenyan case study using artificial intelligence*. Oxford Commission on State Fragility. https://www.theigc.org/wp-content/uploads/2019/02/Language-and-violence-in-Kenya_Final.pdf
- Muji, A. W. and Wahyu, T. D. (2017). The Symbolic Violence in Language. *International Journal of Research in Humanities and Social Studies* Volume 4, Issue 10, 2017, PP 9-15.
- Mwende, S. (2022). Why NCIC banned the term 'Hatupangwingwi'. *The Star*. <https://www.thestar.co.ke/news/2022-04-08-why-ncic-banned-the-term-hatupangwingwi/>
- Ong, W. J. (1982). *Orality and Literacy: The Technologizing of the Word*. New York: Methuen.
- Wardhaugh, R. (2002). *An Introduction to Sociolinguistics. (4th ed)*. Oxford: Blackwell Publishers
- Trudgill, P. (2002). *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society 4th ed*. London: Penguin books.

